JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI
HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA
SHULE YA SEKONDARI
KORONA
S.L.P. 13402, ARUSHA
Barua pepe: koronasecondaryschool2018@gmail.com
SIMU: Mkuu wa Shule 0757745774
Makamu Mkuu wa Shule: 0768909629

KUMB. Na KSS/ADM/JI/2026/01

Bandika picha nusu (passport size) ya Wazazi/Walezi wakiwa pamoja na mtoto hapa	**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi** ....

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KORONA HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA MKOA WA ARUSHA MWAKA 2026/2027**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2026/2027 na atasoma tahasusi ya PCM/CBG/ PGM/PCB. Shule ya Sekondari Korona ipo umbali wa kilometa 17.5 kutoka Arusha Mjini. Usafiri wa basi kutoka mjini Arusha unapatikana Stendi ya kilombero na nauli ni Tshs. 1000/= kwa daladala zinazoelekea Njiro atomic energy, teksi 30,000/= na Bajaji ni tsh 20,000/=
Muhula wa Masomo utaanza kama itakavyo tangazwa na OWM-TAMISEMI.

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

2.1 Sare za Shule

(Mwanafunzi Ajinunulie)

1. Mashati meupe mawili (2) ya mikono mirefu na yasiyo na urembo wowote.
2. Suruali mbili za rangi ya ugoro iliyokolea (dark brown) upana wake iwe na uwezo wa kupanda gotini (isiwe myonyo) na iwe yenye pindo chini.
   -*- Kwa ajili ya kufanana kwa kitambaa mwanafunzi anaweza kuipata shuleni.
3. Sweta rangi ya ugoro (dark brown). Lenye nembo linapatikana shuleni.
4. Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba visivyo na visigino virefu.Ajinunulie
5. Tai rangi ya ugoro (dark brown), yenye mistari mieupe. Inapatikana shuleni
6. Soksi nyeusi jozi mbili. Ajinunulie
7. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia unifomu. Ajinunulie
8. Nguo za michezo, raba nyeusi, bukta nyekundu, T-shirt nyekundu yenye kola. Ajinunulie

9. Track suit ya maroon
10. Shamba dress suruali ya dark blue, upana wake iwe na uwezo wa kupanda gotini (isiwe myonyo) na iwe yenye pindo chini na t-shirt ya maroon yenye kola isiyo na maandishi wala mchanganyiko wa rangi nyingine yoyote itakayowekewa nembo. (*Yenye nembo itapatikana shuleni)*
11. Chandarua nyeupe 1 ya duara na foronya 1 ya godoro la nchi mbili na nusu kwafuti sita na godoro lake, foronya 1 ya mto (rangi ya blue).
12. Nguo za **binafsi (za nyumbani)** haziruhusiwi shuleni kabisa.
13. Wanafunzi wote wanatakiwa wavae sare husika za shule kwa wakati husika.
14. Kila mzazi atagharamia matibabu kwa mwanae, tunashauri mwenye bima ya afya aje nayo na asiyekuwa nayo akatiwe.

2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

1. Rim mbili (2) za karatasi nyeupe A4 (zisizo na mistari), mwanafunzi aje nazo siku ya kuripoti shuleni.
2. Shuka mbili rangi ya bluu zisizo na maua na Blanketi moja (1) zito.
3. Sanduku Ia chuma lenye kufuli imara kwa ajili ya kuhifadhia vifaa.
4. Bakuli, sahani, kikombe na kijiko (visiwe vya plastiki).
5. Ndoo 2 zenye mifuniko(lita 10 moja na lita 20 moja kwa ajili ya kuhifadhia maji).
6. **PCM** walete Kwanja 1, squizer 1, soft bloom 1, **CBG** walete jembe 1, squizer 1, PCB na PGM walete hard bloom 1,reki, squizer 1
7. Madaftari ya kutosha (counter books - 4 quires) zisizopungua 8.
8. Scientific calculator (fx 991E-plus)1, mathematical set 1, Graph pad 2 na spring files 2
9. Dissecting kit 1 imara kwa wanafunzi wanaosoma biolojia.
10. Fomu hii iambatane na nakala ya cheti cha kuzaliwa na nakala ya matokeo ya kidato cha nne (result slip).

2.3 Michango mbalimbali

Shule za Bweni

Na	**Aina ya Mchango**	**Kiasi**
1.	Mchango wa Uendeshaji wa Shule	65,000/=
3.	Tahadhari	5,000/=
4.	Nembo ya mashati	5,000/=
5.	Kitambulisho cha Shule	5,000/=
	Jumla	**80,000/=**

Michango hii ilipwe benki A/C No. 40801200306, NMB.
Mwanafunzi aje na pay-in-slip yenye jina la mwanafunzi husika.

VITABU:

Ifuatayo ni orodha ya vitabu vinavyotumika darasani. Lazima mwanafunzi aje na angalau nakala moja kwa kila somo siku ya kuripoti shuleni.

SOMO	ORODHA YA VITABU
1. ADVANCED MATHEMATICS	• Advanced Level Pure Mathematics, fourth Edition by C.J Tranta • Pure Mathematics I & II - J. K Backhouse • S. Chand - Pure Mathematics class X1 and XII • Understanding P ure Mathematics – A. J. Sadler • Mathematics for advanced secondary school -TIE • Concise course for A'level statistics
2. BASIC APPLIED MATHEMATICS	• Basic Applied Mathematics for Advanced Secondary Schools V and VI – Septine I. Sillem
3. PHYSICS	• Principle of physics XI & XII– S. Chand • Physics for Advanced secondary school - TIE • Understanding Physics - Jim Breclhaupt • Objective of Physics – S. Chand • Mastering Physics I & II- Odasi Charles • Calculation for A Level physics
4. CHEMISTRY 5. Historia ya tanzania na maadili	• Conceptual chemistry XI and XII – S. Chand • Advanced Inorganic Chemistry – Vol I and II – S. Chand • Organic Chemistry Part A & B - Tanzania Publishing House • Physical Chemistry – TIE • Advanced Chemistry – Cambridge low price Edition Philip Mathew. • Historia ya Tanzania na maadili - TIE •
6. GEOGRAPHY	• Landforms in Africa - Colin Buckle • Principles of Physical Geography - Monkhouse • Geography Integrated Approach - Waugh • Practical Geography for Africa - J. M Pritchard • Africa - J. M. Pritchard • Tropical lands - Michael Seniar. • Human and Economic Geography - Morgan. • Geography dictionary • Atlas of Tanzania • The earth's physical environment, physical geography Alive - Zisti Kamili • Advanced level Practical Geography Alive - Zisti Kamili
7. BIOLOGY	• Biological science 4th edition - Taylor • New understanding biology - Glenn & Suzan Toole • Biology - S. Chand
8. Academic communication	• Academic communication - Tie

Mwl. CHRISTOPHER SABAS MALAMSHA

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KORONA

3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu/line/kifaa chochote cha mawasiliano shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kutoroka, kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Saini ya Mkuu wa Shule .....

Jina la Mkuu wa Shule CHRISTOPHER SABAS MALAMSHA

Mhuri wa Mkuu wa Shule MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KORONA

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- **Mkuu wa shule +255757745774**
- **Makamu Mkuu wa Shule +255768909629**
- **Mwandamizi Taaluma +255766098622**
- **Mwandamizi Malezi +255753443876**

FOMU YA KUKUBALI NAFASI NA UTII

1. Mimi……(Jina kamili la **mwanafunzi**), Kidato cha…… mwaka …… natambua wajibu wangu kama mwanafunzi kwa Taifa na jamii kwa ujumla na ninaahidi kwamba:

A. Nitafuata sheria na kanuni zote za shule pamoja na maelekezo yote yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.
B. Nitatii na kuheshimu viongozi wangu wote kuanzia viongozi wa darasa, viranja, watumishi wote wasio walimu na walimu hadi mkuu wa shule.
C. Sitatoka nje ya mipaka ya shule wakati wote nitakapokuwa shuleni labda tu kwa shughuli maalumu na baada ya kupata kibali kwa maandishi kutoka kwa Mwalimu au Mkuu wa Shule mwenyewe.
D. Sitagoma wala kusababisha mgomo wowote kwa kipindi chote nitakapokuwa nikisoma katika shule hii.
E. Kama nitashindwa kufuata hayo yote hapo juu, hatua kali za nidhamu zichukuliwe dhidi yangu ambayo ni pamoja na kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule.

…… …… ……
JINA KAMILI SAINI YA MWANAFUNZI TAREHE

2. Mimi …… **Mzazi / Mlezi**

wa ……

Nimesoma na kuelewa /kukubaliana na sheria na kanuni za shule. Endapo mtoto wangu atashindwa kufuata hayo yote hatua kali dhidi yake zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masorno au kufukuzwa shule.

Pia nitakuwa mwaminifu kutoa ada na michango yote iliyokubaliwa kisheria bila usumbufu na kuhakikisha mtoto wangu anapata mahitaji yote ya muhimu.

NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI ……

…… …… ……
JINA KAMILI LA MZAZI/MLEZI SAINI YA MZAZI/MLEZI TAREHE

3. Mimi ..... (Jina la **mwenyekiti wa mtaa/kijiji)**, Mwenyekiti wa mtaa/kijiji cha .....
nathibitisha kuwa Ndugu .....
ni Mzazi/mlezi wa mtoto huyu aliyechaguliwa kujiunga kidato cha tano.

Maoni/mapendekezo kuhusiana na unavyomfahamu mwanafunzi huyu:
.....
.....

MUHURI

NAMBA YA SIMU .....

....
SAINI YA M/KITI (KIJIJI/MTAA) TAREHE

4. Jina la **Mtendaji Kata** .....
Kata ya .....

MUHURI

NAMBA YA SIMU .....

....
SAINI YA MTENDAJI KATA TAREHE

KORONA SEC SCHOOL
Education for Better Life

HABARI ZA MZAZI / MLEZI

Tafadhali taarifa hizi ni za muhimu sana zijazwe kwa usahihi

1. Jina kamili Ia Baba .....
2. Kazi yake.....
3. Anwani ya mahali pa kazi ya baba .....
   Namba ya simu.....
4. Jina kamili la Mama.....
5. Kazi yake.....
6. Anwani ya mahali pa kazi ya mama.....
   Namba ya simu.....
7. Jina kamili Ia Mlezi (iwapo mtoto haishi na wazazi wake)
   .....
8. Kazi na anwani ya mIezi
   .....
   .....
   .....
9. Nyumbani kwa Baba (alipozaliwa mtoto) Kijiji /Mtaa.....
   Wilaya..... Tarafa .....
   Kata..... Mkoa .....
10. Mtoto anaishi na
    I. Baba tu ☐
    II. Mama tu ☐
    III. Wazazi wote ☐ (*weka alama yay a vema*)
    IV. Walezi ☐
11. Dini ya baba ..... Dhehebu .....
    Dini ya mama ..... Dhehebu .....
    Dhehebu unalotaka mwanao alelewe .....
12. Anwani kamili ya nyumba ambapo mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo
    .....
13. Mimi ..... (Jina la Baba/Mama/Mlezi) wa ..... nathibitisha kuwa taarifa hii hapa juu ni sahihi na naahidi kushirikiana na walimu na uongozi wa shule ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.

....
JINA KAMILI **SAINI** **TAREHE**

PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a medical Officer in Government Hospital in respect of all entrants to Korona Secondary School)

Pupil's full name .....

Age .....

1. Blood count (red and white) .....
2. Stool examinations .....
3. Urinalysis .....
4. Syphilis test .....
5. T.B. test .....
6. Eye test .....
7. Ears test .....
8. Chest .....
9. Abdomen .....
10. Spleen.....
11. Additional information: e.g. physical defect, infection, chronic or family diseases etc

    .....
    .....
    .....
    .....

    Treatment after examination

    .....
    .....
    .....
    .....

(Please state nature of treatment)

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to pursue further studies

Signature .....

Designation .....

Station .....

Date: .....

Official stamp .....